**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA FAMASI**

# TAARIFA KWA UMMA

**UTARATIBU WA KUJIUNGA NA MASOMO YA SHAHADA YA FAMASI**
***(BACHELOR OF PHARMACY DEGREE)***

## 1. UTANGULIZI

Baraza la Famasi ni Taasisi ya Serikali, chini ya Wizara ya Afya iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Famasi, Sura 311. Pamoja na majukumu mengine, Baraza limepewa jukumu la kusimamia taaluma ya famasi na huduma zinazotolewa na wanataaluma wa kada hiyo.

Kifungu Na.4 (i) cha Sheria hiyo kinaekeleza Baraza kushirikiana na mamlaka za ithibati, yaani Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), katika kusimamia na kuhakiki viwango na ubora wa mafunzo ya kifamasia yanayotolewa na vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Kwa mujibu wa **Kanuni Na. 4(1)** ya Kanuni za Elimu na mafunzo za Baraza la Famasi za mwaka 2005, yaani, ***The Pharmacy (Education and Training) Regulations, GN 333 of 2005,*** imeelekezwa kuwa kozi ya Shahada ya Famasi itasomwa kwa kipindi kisichopungua miaka minne (04).

Baraza linapenda kuwakumbusha wanafunzi na watanzania wote wenye nia ya kusoma **ufamasia,** kuzingatia Sheria na Kanuni mbalimbali zinazosimamia taaluma ya famasi nchini. Kwa urahisi wa rejea, **vigezo** husika ni kama vilivyoainishwa kupitia tangazo hili.

## 2. TARATIBU ZA KUDAHILIWA KUSOMA SHAHADA YA FAMASI

Kwa mujibu wa Kanuni ya 31(2) ya Kanuni za vyuo vikuu (*The Universities (General) Regulations, GN 226*) 2013, zipo njia mbili ambazo hutumika wakati wa kudahili wanafunzi wanaoomba kusoma Shahada ya Famasi. Njia hizi ni ile ya moja kwa moja (*Direct entry*) kwa wahitimu wa kidato cha sita (6) na njia ya pili ni ile ya ulinganifu wa vigezo (*equivalent qualification*) kwa wahitimu wa Stashahada (*Diploma*) ya Famasi.

Vilevile, Kanuni ya 31(4) ya Kanuni za vyuo vikuu (*The Universities (General) Regulations, GN 226*) 2013 imeelekeza kuwa, anayeomba kusoma Shahada ya famasi kupitia njia ya ulinganifu wa vigezo (*equivalent qualification*), ni sharti awe amehitimu Stashahada ya famasi na si vinginevyo.

Kadhalika, Kifungu cha **52(2)** cha Sheria ya vyuo vikuu Na.7 ya 2005, kimeelekeza kuwa hakuna muombaji atakayedahiliwa katika masomo ya Shahada, kama hana, au hajatimiza vigezo vilivyowekwa.

## 3. MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KUJIUNGA NA MASOMO YA SHAHADA YA FAMASI

### 3.1: Ndani ya nchi;

Kwa mujibu wa miongozo ya Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU Admission Guidebook*) ambayo hutolewa kila mwaka wakati wa udahili, zipo njia mbili ambazo hutumika kuwadahili wanafunzi wanaoomba kusoma Shahada ya Famasi. Njia hizo ni kama ifuatavyo;

**A. Njia ya moja kwa moja (*Direct entry*)**

Muombaji anapaswa kuwa amehitimu kidato cha sita katika masomo ya sayansi kama ifuatavyo;

**i) Vigezo**

- Awe amesoma masomo ya sayansi yaani Fizikia, Kemia, Baiolojia pamoja na Hisabati na Kiingereza katika kidato cha Nne na kupata alama za ufaulu kwa mujibu wa mwongozo wa TCU (*Admission Guidebook* ) wa mwaka husika.

- Awe amesoma mchepuo wa sayansi yaani masomo ya Fizikia,Kemia na Baiolojia katika kidato cha Sita na kupata alama za ufaulu zinazomruhusu kujiunga na masomo ngazi ya Shahada ya famasi kwa mujibu wa mwongozo wa udahili wa TCU wa mwaka husika.

**B. Kujiunga kupitia vigezo linganifu (*Equivalent qualification*)**

Muombaji anapaswa kuwa amehitimu Stashahada *(diploma)* ya famasi kwa mujibu wa Kanuni ya 31(4) ya Kanuni za *The Universities (General) Regulations, GN 226*) 2013, na kuwa na vigezo vingine kama ifuatavyo;

**i) Vigezo**

- Awe amesoma masomo ya mchepuo wa sayansi katika kidato cha Nne yaani Fizikia, Kemia, Baiolojia, Hisabati pamoja na Kiingereza na kupata alama za ufaulu kwa mujibu wa mwongozo wa TCU (*Admission Guidebook* ) wa mwaka husika.

- Awe amehitimu mafunzo ya Stashahada ya famasi (NTA L6) na kupata ufaulu (GPA) wa kuweza kujiunga na ngazi ya shahada ya famasi kwa mujibu wa mwongozo wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) wa mwaka husika.

## 3.2: <u>Nje ya Nchi</u>

Kwa mwombaji anayependa kusoma Shahada ya Famasi katika vyuo vilivyopo nje ya nchi, utaratibu umeainishwa kupitia Sheria na miongozo mbalimbali kama ifuatavyo;

**A. Muda wa masomo**

Muda wa masomo ya Shahada ya Famasi ni kipindi kisichopungua miaka minne (4) kama ilivyoelekezwa katika **Kanuni Na. 4(1)** ya Kanuni za Elimu na mafunzo za Baraza la Famasi za mwaka 2005 yaani, "*The Pharmacy (Education and Training) Regulations, GN 333 of 2005"*

**B. Vigezo vya kujiunga na masomo**

i Mwombaji anapaswa awe amehitimu kidato cha sita (6) na kufaulu katika masomo ya sayansi yaani Fizikia, Kemia na Baiolojia kwa mujibu wa mwongozo wa TCU (*TCU Admission Guidebook*) wa mwaka husika

ii Mwombaji anapaswa awe amesoma masomo ya mchepuo wa sayansi katika kidato cha nne yaani Fizikia, Kemia, Baiolojia na amehitimu kozi ya famasi katika ngazi ya Stashahada *(diploma)* kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 31(4) ya Kanuni za vyuo vikuu (*The Universities (General) Regulations, GN 226*) za Mwaka 2013;

**C. Utaratibu wa kuomba udahili**

**i) Kupata maelekezo na ushauri kutoka Baraza la Famasi**

Kwa mujibu wa mwongozo wa TCU (*Principles and Guidelines for Licensing Overseas Student Recruitment Agencies and issuance of a* ***No Objection Certificate***) wa Desemba 2019, Kanuni ya **sita (6)** mwongozo **wa 6.1,** mwombaji anaekusudia kutoa huduma za kitaaluma baada ya kuhitimu masomo ya Shahada ya Famasi nje ya Nchi, anapaswa kufika Ofisi za Baraza la Famasi ili kupata maelekezo na ushauri kabla ya kupata ***NOC*** juu ya;

- Kozi anayokusudia kusoma,
- Vigezo vinavyohitajika.
- Chuo anachoenda kusoma
- Umahiri anaopaswa kuwa nao ili atakapohitimu aruhusiwe kutoa huduma za dawa nchini Tanzania.

***ii)*** **Kupata *No Objection Certificate (NOC)***

Baada ya kupata ushauri wa kitaaluma kutoka Baraza la Famasi, mwombaji anapaswa kupata cheti *(NOC)* kitakachomruhusu kupata elimu ya juu nje ya Nchi kutoka TCU. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 5 mwongozo wa 5.1 wa *Principles and Guidelines for Licensing Overseas Student Recruitment Agencies and issuance of a No Objection Certificate*) wa Desemba 2019.

## 4. UTARATIBU BAADA YA KUHITIMU MASOMO

### 4.1 Tathmini ya nyaraka za wahitimu -TCU

Baada ya kuhitimu masomo na kutunukiwa Shahada ya Famasi, muhitimu anawasilisha nyaraka zake TCU ili Tume ijiridhishe juu ya uhalali wa nyaraka hizo. Hii ni pamoja na vigezo vya udahili kama vilizingatia taratibu zote.

Kwa mujibu wa kanuni ya Pili (2), mwongozo wa 2.1 (b) wa kanuni za *Evaluation of Foreign Awards and Recognition of Qualifications* za Desemba 2019, endapo itaonekana vigezo vya nchi husika vinakinzana na vigezo vya hapa nchini, vigezo vya Tanzania vitazingatiwa.

### 4.2 Tathmini ya nyaraka za wahitimu - Baraza la Famasi

Kadhalika Kanuni ya Tano (5) mwongozo wa 5.2 wa kanuni za ***Evaluation of Foreign Awards and Recognition of Qualifications*** za Desemba 2019, inasisitiza kuwa baada ya muhitimu kupata cheti cha utambuzi wa Shahada yake kutoka TCU (*Certificate of Recognition*), anapaswa kuwasilisha nyaraka zake katika Ofisi za Baraza la Famasi ili kutathmini umahiri wa muhitimu kitaluuma na kupata idhini ya kutoa huduma za kitaaluma nchini Tanzania.

## 5. MWISHO

Tangazo hili limetolewa kwa nia ya kuwakumbusha na kuwaasa watanzania wote wenye nia ya kusoma ufamasia kuhakikisha wanafuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa. Hii itasaidia kuepusha usumbufu wakati wa usajili wa wanataaluma kwani Sheria na Kanuni hizi zimekuwepo tangu Mwaka 2005. Kadhalika Baraza linawakumbusha kuzingatia vigezo husika kama vinavyotolewa na TCU mwaka hadi mwaka.

Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe *info@pc.go.tz* au simu namba 0736222515.

Imetolewa 10 Machi, 2025 na;

**Boniface M. Magige**
**MSAJILI**
**BARAZA LA FAMASI**